

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE  
NA WATOTO



HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA WA SIMIYU

MKATABA NAMBA: MOHCDGEC/SRRH/2021/2022/W/01

WA

FUNDI MJENZI WA JENGO LA WAGONJWA WA DHARURA (EMD)

KATI YA

WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA  
WATOTO

S.L.P 743,  
DODOMA.

NA

WAKALA WA MAJENGO TANZANIA (TBA-SIMIYU)

S.L.P 159,  
BARIADI.

NOVEMBA, 2021

AP

## **1. FOMU YA MKATABA**

A handwritten signature in black ink, consisting of stylized, overlapping loops and a long horizontal stroke extending to the right.



**FOMU YA MKATABA**

Mkataba huu umefungwa leo .....27, Novemba, 2021.....kati ya

**Katibu Mkuu, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto wa S.L.P 743 Dodoma** kwa upande mmoja

na

**Meneja, Wakala wa Majengo Mkoa wa Simiyu wa S.L.P 159 BARIADI** (Hapa ataitwa "Mkandarasi") kwa upande mwingine.

Kwa kuwa Mwajiri anataka baadhi ya kazi zifanyike yaani: Ujenzi wa Jengo la Wagonjwa wa Dharura katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Simiyu (Nyaumata) na kwa barua ya kukubali yenye Kumbukumbu namba **GC:109/590/II/01/45** ya tarehe 26 Novemba, 2021 alikubali zabuni ya Mkandarasi/Fundi Sanifu (Local Fundi) kwa utekelezaji na ukamilishaji wa kazi hiyo.

**SASA MAKUBALIANO HAYA YAMESHUHUDIWA KAMA IFUATAVYO:**

1. Katika makubaliano haya maneno na maelezo yatakuwa na maana sawa kama yalivyopewa katika masharti ya mkataba unaorejelewa na;
2. Nyaraka zifuatazo zitachukuliwa kwa pamoja na zisomeke na kufasiriwa kuwa ni sehemu ya makubaliano haya, yaani:-
  1. Fomu ya Mkataba;
  2. Barua ya kukubali Kotesheni;
  3. Fomu ya kuwasilisha Kotesheni;
  4. Masharti maalumu ya Mkataba;
  5. Masharti ya jumla ya Mkataba;
  6. Uainishaji viwango na vipimo;
  7. Michoro;
  8. Mchanganuo wa makadirio ya kazi;
  9. Mchanganuo wa makadirio Vifaa vya ujenzi
  10. Nyaraka nyingine zozote zinazounda sehemu ya mkataba (Kumbukumbu za ufafanuzi, memoranda dhidi ya rushwa).
3. Nyaraka zote zilizotajwa hapo juu zitarejelewa hapo baadae kama 'Mkataba' na





zitachukuliwa kuwa zinakamilishana na zinajieleza sawa lakini ukitokea utata au uhitilafiano zitakuwa na umuhimu katika mfuatano wake kama zinavyoonyeshwa hapo juu.

4. Katika kuzingatia malipo yanayofanywa na Mwajiri kwa Mkandarasi kama baadaye inavyotajwa, Mkandarasi hapa anakubaliana na Mwajiri kutekeleza na kukamilisha kazi kwa kufuata makubaliano, kwa hali zote kulingana na vifungu vya mkataba.

Mwajiri hapa anakubali kumlipa Mkandarasi kwa kuzingatia utekelezaji na ukamilishaji wa kazi, jumla ya fedha za Tanzania milioni mia moja thelathini na sita, laki mbili thelathini na sita na thelathini na saba tu (TZS 136,236,037.00) baadaye imerejelewa kama 'Bei ya Mkataba' kwa nyakati na namna iliyoelezwa katika mkataba.

**KATIKA KUSHUHUDIA**, pande hizi zimekubaliana na kutia Saini na muhuri katika siku na mwaka kama ulivyoandikwa hapo juu.

**IMETIWA SAINI KWA NIABA YA MWAJIRI**

MGANGA MFAWIDHI  
HOSPITALI YA RUFAA  
YA MKOA - SIMIYU

Mbele ya

Saini

(Jina) DR. MIKE MABIMBI

(Cheo) MGANGA MFAWIDHI

Saini

(Jina) DICKSON RUKANANDA

(Cheo) AFLA SHERIA

**KWA NIABA YA MKANDARASI/FUNDI SANIFU:**

MENEJA WA MKOA  
WAKALAWA MAJENGO TANZANIA  
S.L.P 159  
BARIADI - SIMIYU

Mbele ya

Saini

(Jina)

(Cheo)

Saini

(Jina)

(Cheo)



## **2. BARUA YA KUKUBALI KOTESHENI**

AP

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA SIMIYU  
Anwani ya Simu: "REGCOM"  
Simu Na: 028-2700011/2700054  
Nukushi: 028-2700168  
Barua pepe: [ras@simiyu.go.tz](mailto:ras@simiyu.go.tz)



OFISI YA MKUU WA MKOA,  
S.L.P. 4,  
BARIADI.

**Kumb Na. GA124/134/01G/....**

23 Novemba, 2021

WAKALA WA MAJENGO TANZANIA (TBA)  
S.L.P 159,  
BARIADI,  
SIMIYU.

**YAH: UJENZI WA JENGO LA WAGONJWA WENYE UANGALIZI MAALUM (ICU),  
WAGONJWA WA DHARURA NA NYUMBA YA MTUMISHI KATIKA HOSPITALI YA  
RUFEE YA MKOA WA SIMIYU KWA MWAKA 2021/2022**

**SOMO: KUKUBALI KOTESHENI YA GHARAMA YA UFUNDI YA UJENZI WA  
JENGO LA WAGONJWA WA DHARURA (EMD)**

Husika na mada tajwa hapo juu,

2. Hii ni kukutaarifu kuwa kotesheni yako ya tarehe **15/11/2021** ya kufanya kazi ya Ujenzi wa JenGO la Wagonjwa wa Dharura (EMD) katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Simiyu kwa bei ya Mkataba wa shilingi za Tanzania **Millioni Mia Moja Thelathini na Sita, Laki Mbili elfu Thelathini na Sita na Thelathini na Saba tu (TZS 136,236,037.00)** kama ilivyosahihishwa na kurekebishwa kulingana na maelekezo ya mwaliko wa kotesheni imekubaliwa.
3. Unatakiwa kuthibitisha kwa barua tuzo hii mara baada ya kupokea barua.
4. Aidha unatakiwa kuweka sahihi ya makubaliano ya Mkataba tarehe **27/11/2021** muda wa **saa tatu na nusu asubuhi** na uanze kazi katika muda wa **wiki moja** kutoka siku mkataba utakapotiwa saina.
5. Nashukuru kwa ushirikiano

P.J. Kayombo

KATIBU TAWALA MKOA  
SIMIYU



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI  
**WAKALA WA MAJENGO TANZANIA**

Anwani ya Simu " **MAJENGO**" Simiyu  
Simu: 028-2700088  
Nukushi: 028-2700111  
BaruaPepe: [rm.simiyu@tba.go.tz](mailto:rm.simiyu@tba.go.tz)  
Tovuti : [www.tba.go.tz](http://www.tba.go.tz)



Ofisi ya Meneja wa Mkoa,  
S.L.P. 159,  
Bariadi-Simiyu,  
**TANZANIA**

Unapojibu tafadhali taja:

**26/11/2021**

**Kumb Na. GC:109/590/II/01/44**

Katibu Tawala wa Mkoa,  
Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,  
S. L. Posta 4,  
**BARIADI - SIMIYU.**

**YAH: UJENZI WA JENGO LA WAGONJWA WENYE UANGALIZI MAALUM  
(ICU) KATIKA HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA WA SIMIYU.**


**Somo: Kukubali Zabuni ya Nguvu Kazi**

Tafadhali rejea somo tajwa hapo juu.

Ofisi ya Wakala wa Majengo Tanzania Mkoa wa Simiyu imekubali Zabuni ya Nguvu Kazi katika Ujenzi wa Jengo la Wagonjwa wenye Uangalizi Maalum (ICU) katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Simiyu kwa Mkataba wa **TZS.123,835,779.32 (Shilingi za Tanzania Milioni Mia Moja Ishirini na Tatu Mia Nane Thelathini na Tano Eflu Mia Saba Sabini na Tisa na Senti Thelathini na Mbili tu)** Pamoja na Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa muda wa Miezi Minne (4).

Asante sana kwa kutupatia kazi hii na tunaahidi kuifanya kwa umahiri na Weledi Mkubwa.

Wako katika Ujenzi wa Taifa.

  
Eng. Abubakar A. Abdulkhanna  
**KAIMU MENEJA WA MKOA**  
WAKALA WA MAJENGO TANZANIA  
S.L.P. 159  
BARIADI - SIMIYU

### **3 FOMU YA KUWASILISHA KOTESHENI**

A handwritten signature in black ink, located in the bottom left corner of the page. The signature is stylized and appears to be a combination of letters, possibly 'AF' or 'AFI'.



FOMU YA KUWASILISHA NUKUU YA BEI

Tarehe: 15/11/2021

Kwa: KATIBU TAWALA MKOA

S.L.P 4,

BARIADI SIMIYU

Tunaahidi/ Naahidi kutekeleza kazi ya MoHCDGEC/SRRH/2021/2022/W/01 kulingana na

Masharti ya Mkataba yanayofuatana na Nukuu za Bei ya Mkataba ya  
Upiza wa Jengo la Wagaji wa Dhoru (EMD) kwa Shilingi  
za Tanzania Mitoni Mili Moja thekethu na Sita Mili mbili thekethu na Sita  
Ene na thekethu na Sebe tu - TZS 136,236,037/- tarakimu na aina ya  
[ingiza kiasi katika maneno, ...] sarafu] Shilingi za Tanzania.

Pia tunaahidi kukamilisha kazi iliyotajwa katika kipindi cha miezi MINNE (4)(), ambacho  
kinajumuisha kipindi cha maandalizi.

Nukuu za Bei hii pamoja na barua yako ya kukubali kwa maandishi vitafanya mkataba  
unaotufunga sisi pamoja. Tunafahamu kuwa hulazimiki kukubali kiwango cha chini au  
kotesheni yoyote kati ya kotesheni unazopokea.

Tunathibitisha kuwa kotesheni hii imetimiza masharti kama yanavyotajwa katika Mwaliko wa  
Nukuu za Bei.

Sahihi Idhinishwa: .....

Jina na Cheo cha Mweka Sahihi: .....

Jina la Fundi: KAINU X ... WA MKOA

MENEJA WA MKOA  
WAKALAWA MAJENGO TANZANIA  
S.L.P 159  
BARIADI - SIMIYU

Eng. ABUBAKAR A. SHEKATW

#### **4. MASHARTI MAALUMU YA MKATABA**

A handwritten signature in black ink, consisting of a stylized 'S' followed by a vertical line and a small dot.



## **MASHARTI MAALUMU YA MKATABA**

Taarifa maalumu ifuatayo kwa ajili ya kazi inayofanywa itakuwa nyongeza, au inaweza kurekebisha vifungu katika Masharti ya Jumla ya Mkataba. Kunapokuwa na mgogoro, vifungu katika **Masharti Maalumu ya Mkataba** vitakuwa na nguvu zaidi ya vifungu katika **Masharti ya Jumla ya Mkataba**.



Masharti Maalumu ya Mkataba Kifungu Na;	Masharti ya Jumla ya Mkataba Kifungu Na;	Marekebisho ya, na Nyongeza kwa vifungu katika Masharti ya Jumla ya Mkataba.
1	04	Kiswahili/Kiingereza
2	07	Zana,mitambo na vitendea kazi vya mafundi vitatolewa na mkandarasi isipokuwa gharama za maji, ulinzi na umeme
3	16	Mkandarasi atawajibika kuhakikisha ubora wa maunzi anazopewa zinakidhi vigezo/viwango vya kitalaamu.gharama ya upimaji wa maunzi itakuwa ya mshitiri.
4	17	Mkandarasi atatoa makadirio ya maunzi anayoyahitaji kwa kila hatua ya utekelezaji, mkandarasi na mshitiri watapitia kwa pamoja kabla ya kuagiza maunzi.
5	20.0	Mkataba utanza tarehe: 1 /12/2021 na kukamilisha kazi kwa muda wa miezi minne, ifikapo 31/3/2022
6	23.1	Malipo ya awali ni 20% ya bei ya Mkataba. Malipo mengine yatalipwa kwa hati ya madai isiyopungua asilimia ishirini ya mkataba wa nguvu kazi.  Marejesho ya Malipo ya awali yatakuwa ni asilimia ishirini ya hati ya malipo iliyoombwa.
7	23.2	Fedha itakayoshikiliwa ni asilimia mbili (2.% )ya thamani ya cheti cha malipo. (rentation)
8	23.4	Kiwango cha riba kwa kiasi kisicholipwa, kitalipwa endapo mshitiri atachelewesha malipo kwa makusudi kitakuwa sawa na kile kiwango cha riba kwa mwezi kinachotumiwa na benki ya biashara kama kilivyopitishwa na Benki Kuu ya Tanzania tarehe ya kutia sahihi mkataba. <b>[hakihusiki]</b>
9	26.0	Kiasi cha kulipia ucheleweshaji kazi: <b>[hakihusiki]</b>



## **5.MASHARTI YA JUMLA YA MKATABA**

A handwritten signature in black ink, consisting of stylized, overlapping loops and lines.

**A: VIFUNGU JUMLA**

**Kifungu 1: Nyaraka za Mkataba**

Masharti ya Mkataba na fomu ya Maelezo ya mahitaji, Viwango na vipimo ni sehemu muhimu ya nyaraka za Mkataba na zinapaswa kusomwa pamoja na nyaraka nyingine zote zinazounda Mkataba. Kama ikitokea kunaonekana kuna mgogoro kipaumbele cha nyaraka kitakuwa kama ilivyoainishwa katika **Kifungu cha 6** cha Masharti ya Mkataba.

**Kifungu 2: Tafsiri**

Katika haya Masharti ya Mkataba, maneno yafuatayo yatakuwa na maana zilizotolewa kwa maneno hayo kama ilivyo hapa chini:

**Mwajiri:** Katibu Mkuu, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

**Mhandisi:** Mtu aliyeteuliwa na Mwajiri na kuwa na wajibu wa usimamizi wa kazi na usimamizi wa mkataba

**Mwakilishi wa Mhandisi:** Mtu aliyeteuliwa na Mhandisi Mwenye wajibu wa Kusimamia Kazi.

**Mkandarasi** Mtu au watu au kampuni ambayo zabuni yao imekubaliwa na Mwajiri.

**Kazi** Ni Kazi zinazotakiwa kufanywa kulingana na mkataba.

**Kifungu 3: Maelekezo**

Maelekezo yanayotolewa na Mhandisi yatakuwa kwa maandishi. Ikiwa kwa sababu nyingine yoyote ile maelekezo hayo yatatolewa kwa mdomo, Mkandarasi atafuata maelekezo hayo. Katika kipindi cha **siku 7** maelekezo hayo ya mdomo yatathibitishwa kwa maandishi.





#### **Kifungu 4: Lugha**

Notisi zote, maelekezo na mawasiliano au waraka wowote wa maandishi unaohusu mkataba utakuwa kwa Kiswahili kadiri itakavyokubaliwa na pande zote ilimradi, nyaraka zote zinazotolewa kuhusiana na mkataba unaotekelezwa kwa ushirikiano wa fedha za mkopo au ruzuku zitaandikwa kwa Kiingereza.

#### **Kifungu 5: Sheria inayotumika**

Mkataba, maana yake, fasiri yake, na utekelezaji wake vitaongozwa na Sheria ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

#### **Kifungu 6: Nyaraka za Mkataba zenye Kipaumbele**

Nyaraka kadhaa zinazofanya mkataba zichukuliwe kuwa zinajieleza kikamilifu lakini kama ikitokea hitilafu yoyote ile nyaraka zenye umuhimu wa kwanza zitakuwa zifuatazo:-

1. Fomu ya Mkataba;
2. Barua ya kukubali Kotesheni;
3. Fomu ya kuwasilisha Kotesheni;
4. Masharti maalumu ya Mkataba;
5. Masharti ya jumla ya Mkataba;
6. Uainishaji viwango na vipimo;
7. Michoro;
8. Mchanganuo wa makadirio ya kazi;
9. Mchanganuo wa makadirio Vifaa vya ujenzi
10. Nyaraka nyingine zozote zinazounda sehemu ya mkataba ( Kumbukumbu za ufafanuzi, memoranda dhidi ya rushwa).





## **B: MAJUKUMU**

### **Kifungu 7: Utekelezaji wa Kazi**

Mkandarasi atatoa nguvu kazi, zana, mitambo, usafiri, vifaa na chochote kile kinachohitajika kwa ukamilishaji wa kazi ikiwa ni pamoja na maji na umeme. Atafanya kazi kulingana na inavyotakiwa na nyaraka za mkataba, na maelekezo ya ziada kama yatakavyotolewa mara kwa mara.

### **Kifungu 8: Hali Mbaya ya Ukinzani**

Iwapo wakati wa utekelezaji wa kazi Mkandarasi atapambana na hali mbaya ya ukinzani ambayo haihusiani na hali ya hewa na ambayo haikuwa imetabiriwa na Mkandarasi, Mhandisi atatathimini kuongeza muda ambao Mkandarasi anastahili.

### **Kifungu 9: Kutoa kazi kwa Mkandarasi Msaidizi**

Mkandarasi hatatoa kazi au sehemu ya kazi kwa Mkandarasi msaidizi bila kibali cha maandishi cha kutoka kwa Mwajiri. Kibali kama hicho kinapotolewa hakimwondolei Mkandarasi mamlaka au majukumu yake chini ya maktaba na hivyo Mkandarasi atakuwa na wajibu kwa kushindwa au kuzembea kwa Wakandarasi wasaidizi.

### **Kifungu 10: Usimamizi wa Kazi Unaofanywa na Mkandarasi**

Mkandarasi atatekeleza kazi kwa uangalifu na kwa kufuata utendaji unaotakiwa na Mhandisi ili kufikia mahitaji maalumu ya ubora, kiasi na muda uliopangwa. Kama katika wakati wowote ule Mhandisi anaona uzembe, au kubadilika sana kwa mwelekeo wa programu, hatua zinazofaa zitachukuliwa na Mkandarasi ili kurekebisha hali.

### **Kifungu 11: Ukaguzi**

Mhandisi au mwakilishi wake aliyempa mamlaka ana haki ya kukagua kazi na Mkandarasi atatoa usaidizi kwa shughuli hiyo na kwa wakati Mhandisi atakapohitaji





**Kifungu 12: Kazi Zinazokataliwa**

Kazi ambazo hazikuzingatia masharti ya mkataba zitakataliwa. Kwa maelekezo ya Mhandisi, Mkandarasi kwa gharama zake mwenyewe atatengeneza au kurekebisha au kufanya upya kazi itakayokataliwa hadi kumridhisha Mhandisi.

**Kifungu 13: Bima**

Mkandarasi ataweka bima yenye jina lake na Mwajiri kwa ajili ya hasara au uharibifu wa zana, vifaa na mitambo ya Mkandarasi na pia kwa kufidia majeruhi au vifo.

**Kifungu 14: Wajibu wa Mkandarasi**

Mkandarasi hatamhusisha Mwajiri dhidi ya madai yoyote yanayotokana na hasara au uharibifu wa upande wa tatu (third party). Atamkinga kikamilifu Mwajiri wake dhidi ya madai au hasara zitakazotokana na Sheria ya Ajira na Fidia ya Wafanyakazi.

**Kifungu 15: Jambo Lisilo zuilika**

Katika tukio la hasara yoyote au uharibifu unaotokea katika utendaji wa aina yoyote wa nguvu za asili ambao pande za mkataba hazikuweza kufikiria mapema, Mkandarasi atarekebisha hasara au uharibifu. Mwajiri ataaamua kutoa ziada ya Bei ya Mkataba na pia anaweza kufikiria kutoa muda wa nyongeza wa kipindi cha mkataba.

**Kifungu 16: Ubora wa Maunzi na Usanifu wa Kazi**

Maunzi yote na usanifu wa kazi vitakuwa na ubora kama ilivyofafanuliwa katika mkataba na pia kulingana na maelekezo ya Mhandisi na vitapimwa kama Mhandisi atakavyoona inafaa. Mkandarasi atatoa bure msaada unaohitajika kwa ajili ya kupima ubora wa maunzi na atakuwa na wajibu wa kugharimia upimaji wote utakaohitajika.





**Kifungu 17: Upatikanaji wa Maunzi**

Mkandarasi atabainisha vyanzo vyote vya maunzi yanavyohitajika kabla ya kuanza kazi. Mwajiri akitakiwa anaweza kuwezesha upatikanaji wa vyanzo hivyo. Mkandarasi hatatumia maunzi bila kupata kibali cha maandishi kutoka kwa Mhandisi.

**Kifungu 18: Usafishaji wa Eneo la Kazi**

Baada ya kumaliza kazi, Mkandarasi ataondoa kutoka eneo la kazi zana zote, na maunzi ya ziada, uchafu na mitambo ya muda na ataacha eneo la kazi likiwa safi na katika hali itakayokubaliwa na Mhandisi.

**Kifungu 19: Afya, Usalama na Kulinda Mazingira.**

Mkandarasi katika kipindi chote cha mkataba atakuwa na wajibu kamili wa kiafya na kiusalama katika eneo lake la kazi na watu wote wanaopaswa kuwa katika eneo la kazi katika hali ya mpango mzuri ili kuepusha hatari kwa watu hao. Mkandarasi atazingatia mahitaji na kanuni zote za mazingira kama zinavyoelezwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Kifungu 20: Kuanza na Kukamilika kwa Kazi.**

Mkandarasi ataanza na kukamilisha kazi katika muda uliyoelezwa kwenye Masharti Maalumu ya Mkataba au katika kipindi cha mkataba cha nyongeza, kama kipindi hicho kimeruhusiwa na Mwajiri.

**Kifungu 21: Mabadiliko ya Wigo wa kazi**

Kwa idhini ya Mwajiri, Mhandisi anaweza kubadilisha umbo, ubora au kiasi cha kazi na atakuwa na mamlaka ya kumwagiza Mkandarasi ipasavyo. Mabadiliko hayo yatafanywa kwa agizo la Mabadiliko katika Mkataba. Mhandisi ataamua kuhusu kiasi (kama itatokea) ambacho kwa maoni yake kinapaswa kuongezwa au kupunguzwa kutoka jumla ya fedha iliyotajwa kwenye Mkataba kwa ajili ya kazi yoyote ya nyongeza iliyofanywa au iliyoachwa kwa agizo hilo. Kiasi cha fedha kitakachoamuliwa kitatokana na





kiwango cha kizio au kama hakuna kiwango cha kizio kinachotumika, kiwango kingine kitatumika kama itakavyoamriwa na Mhandisi na kukubaliwa na wote, Mwajiri na Mkandarasi.

## **C: MALIPO**

### **Kifungu 22: Kiasi**

Kiasi kilichowekwa kwenye mchanganuo wa Makadirio ya Kazi ni kiasi kilichokadiriwa kwa kazi na kisichukuliwe kuwa ndiyo kiasi halisi sahihi kitakachofanywa na Mkandarasi. Mhandisi atapima thamani ya kazi halisi iliyofanyika na ataidhinisha gharama halisi ya kazi iliyofanyika kama ilivyofafanuliwa katika mkataba. Ukomo wa kiasi cha kazi unaweza kuongezeka au kupungua kwa asilimia 10 ya bei ya mkataba na hii haitahitaji kibali cha Bodi ya Zabuni.

### **Kifungu 23: Malipo**

#### **23.1 Malipo ya Awali**

Malipo ya Awali ya **asilimia 15** ya thamani ya mkataba **yanaweza** kutolewa kama itakuwa inaonyesha hivyo kwenye **Masharti Maalumu ya Mkataba** baada ya kuwasilisha dhamana ya malipo wali inayokubalika. Malipo ya awali yatakatwa kwa mafungu katika madai yatakayowasilishwa na Mkandarasi kwa malipo, mpaka malipo ya awali yote yatakaporudishwa kikamilifu.

#### **23.2 Malipo Wakati Kazi Inaendelea**

Malipo yatafanywa kwa Mkandarasi wakati kazi inaendelea baada ya Mhandisi kutoa cheti kinachoonesha kuwa kazi imekamilika kwa viwango vilivyoainishwa kwenye mkataba. Katika kila cheti mwajiri atashikilia kiasi kilichotajwa katika Masharti Maalum ya Mkataba na kisichozidi asilimia kumi ya bei mkataba. Fedha hiyo iliyoshikiliwa italipwa katika cheti cha





malipo ya mwisho. Kiasi cha fedha anachodai Mkandarasi kitalipwa na Mwajiri kwa Mkandarasi katika kipindi cha **siku 28 za kazi** baada ya idhini ya cheti cha malipo kutolewa na Mhandisi.

### **23.3 Malipo ya Mwisho**

Cheti cha malipo ya mwisho kitatolewa ndani ya siku **28** za kazi baada ya nyaraka hiyo kuidhinishwa na Mwajiri, ilimradi kazi zote, marekebisho yote na matengenezo yote kama yapo yatakuwa yametekelezwa na hivyo mhandisi kuridhika.

### **23.4 Ucheleweshwaji wa Malipo**

Kama mwajiri atashindwa kufanya malipo katika muda uliotajwa, Mwajiri atamlipa Mkandarasi riba katika kiwango kilichotajwa kwenye **Masharti Maalumu ya Mkataba**.

### **23.5 Makato ya Malipo**

Mwajiri atakuwa na haki ya kukata fedha kiasi cho chote, fedha ya awali au madeni yanayolipika kutoka kwa Mkandarasi kwenda kwa Mwajiri kutokana na fedha yoyote anayoweza kulipwa Mkandarasi na Mwajiri chini ya mkataba huu au mkataba mwingine ilimradi kifungu hiki hakitaathiri marekebisho yoyote kwa amri ya sheria au pengine Mwajiri anaweza kuwa na haki ya kurudishiwa fedha yoyote kama hiyo.

### **23.6 Malipo kwa Wafanyakazi**

Kama kutatokea kushindwa kulipa mishahara/ujira na fidia nyingine zinazopaswa kulipwa wafanyakazi na /au malipo ya kukodisha mitambo/zana/magari na vifaa chini ya mkataba huu, mwajiri atakuwa na haki ya kushikilia malipo ya Mkandarasi.

Mwajiri atatumia fedha alizoshikilia kuwalipa wafanyakazi wa Mkandarasi mishahara yao na fidia nyingine na ada za kukodisha maunzi. Malipo kama hayo yatachukuliwa kuwa ni malipo yaliyopokelewa na Mkandarasi kutoka kwa Mwajiri chini ya mkataba huu.





#### **Kifungu 26: Malipo ya Ucheleweshaji kazi**

Kama Mkandarasi atashindwa kukamilisha kazi yake katika muda uliotajwa kwenye mkataba au katika muda wote wa nyongeza ulioruhusiwa na Mwajiri, Mkandarasi atamlipa Mwajiri malipo ya ucheleweshaji wa kazi katika kiwango cha asilimia 0.1 cha thamani ya mkataba kwa siku mpaka kiwango cha juu cha asilimia 10 ya bei ya mkataba

#### **D: KUSULUHISHA MIGOGORO NA KUVUNJA MKATABA**

##### **Kifungu 27: Kusuluhisha Migogoro**

Kama migogoro ikitokea itasuluhishwa kwa majadiliano ya pande zote. Kama mazungumzo yatashindwa kuleta makubaliano, kila upande una hiari ya kwenda kwenye maamuzi kulingana na sheria za Tanzania.

##### **Kifungu 28: Uvunjaji wa Mkataba**

28.1 Kama Mkandarasi anashindwa kuanza kazi katika muda uliopangwa au kuna sababu ya kutosha kuwa hatakamilisha kazi katika muda uliopangwa au kuna ucheleweshaji uliokiuka tarehe ya kukamilisha kazi au hayuko makini kufuata maelekezo yanayotolewa na Mhandisi au anakuwa mufilisi, Mwajiri atakuwa na haki ya kuvunja mkataba na kumwajiri Mkandarasi mwingine kufanya kazi hiyo.

28.2 Kama Mwajiri atashindwa kumlipa Mkandarasi katika muda wa siku 60 tangu tarehe ya cheti cha malipo kuidhinishwa na Mhandisi, Mkandarasi anaweza kuvunja mkataba.

##### **Kifungu 29: Malipo kama Mkataba Umevunjwa**

Kama mkataba utavunjwa, Mkandarasi atalipwa na Mwajiri kiasi cha fedha au vifaa ambavyo havitakuwa tayari vimelipiwa katika malipo



yaliyofanywa kwa Mkandarasi kwa kazi zote zilizofanywa kabla ya tarehe ya kuvunjwa kwa mkataba kwa kiwango na bei inayotolewa kwenye mkataba. Kila malipo yoyote yanayofanywa na Mwajiri chini ya kifungu hiki, mwajiri atakuwa na haki ya kulipwa madeni yote kutokana na malipo ya awali aliyolipwa Mkandarasi kwa ajili ya mitambo/zana/magari na maunzi na jumla yoyote ya fedha ambayo imelipwa hapo awali na Mwajiri kwenda kwa Mkandarasi kwa minajiri ya utekelezaji wa kazi.





## **6. UAINISHAJI VIWANGO NA VIPIMO**

**(IMEUNGANISHWA PEKEE) SEPARATE BINDED**

A handwritten signature in black ink, consisting of stylized, overlapping loops and lines, located in the bottom left corner of the page.

**7. MICHORO**

A handwritten signature or mark, possibly a stylized 'P' or 'R', located at the bottom left of the page.



## **7. MCHANGANUO WA MAKADIRIO YA KAZI**

A handwritten signature in black ink, consisting of stylized, overlapping loops and strokes, located in the bottom left corner of the page.



# GHARAMA ZA UFUNDI UJENZI WA HOSPITALI YA RUFAA YA SIMIYU (SRRH)

## JENGO LA EMERGENCY DEPARTMENT (EMD)

Na	AINA YA KAZI	BEI YA UFUNDI
1	<b>Msingi wa Jengo (sub structure)</b>	
i	Kuseti jengo	1,723,515.816
ii	Uchimbaji wa msingi pamoja na shimo za nguzo	4,572,659.877
iii	Kufukia na kushindilia msingi	1,436,263.180
		7,732,438.871
<b>B</b>	<b>Usukaji wa nondo katika</b>	
i	Kitako cha nguzo (column base)	574,505.272
ii	Nguzo wa wima za msingi (column starter)	574,505.272
iii	Nguzo mlalo za kwenye msingi (Ground beam)	861,757.1908
iv	Uwekaji wa BRC Mesh eneola jamvi	430,818.1954
v	Strip foundation	1,105,639.6971
		3,547,287.101
<b>C</b>	<b>Kufunga na kuondoa mbao</b>	
i	Pembezoni mwa jamvi	789,917.5021
ii	Pembezoni mwa nguzo wima za msingi, pembezoni mwa nguzo mlalo za msingi pamoja na pembeni mwa kitako cha nguzo (column base)	5,704,716.852
		6,494,644.351
<b>D</b>	<b>Kumwaga zege</b>	
i	Chini ya kitako cha msingi kwa ajili ya kupokea nondo za strip foundation	1,476,714.803
ii	Chini kwenye kitako cha msingi (strip foundation)	3,274,680.050
iii	Chini kwenye kitako cha nguzo (blinding) na kwenye kitako cha nguzo (column base)	1,382,308.7291
iv	Katika nguzo wima za awali (column starter)	507,701.8271
v	Katika nguzo mlalo za kwenye msingi (ground beam)	941,411.975
vi	Kwenye jamvi (oversite concrete)	5,566,956.7251
vii	Umwagiliaji maji	1,927,263.7251
	<b>JUMLA NDOGO</b>	15,077,037.701

MENEJA WA MKOA  
WAKALA WA MAJENGO TANZANIA  
S.L.P 159  
BARIADI - SIMIYU



Na	AINA YA KAZI	BEI YA UFUNDI
<b>A</b>	<b>Kuta za msingi</b>	
i	Ujenzi wa kuta za msingi	3,267,485.110
		3,267,485.110
<b>B</b>	<b>Upangaji na ushindiliaji</b>	
i	Upangaji wa mawe nautandazaji wa DPM	2,929,976.884
ii	Uwekaji wa kifusi nakushindilia katika misingi, mashimo ya nguzo na na kwenye jamvi	1,149,010.544
iii	Uwekaji wa sumu ya mchwa	143,626.318
		4,222,613.75
	<b>JUMLA KATIKA MSINGI WA JENGO (SUB STRUCTURE)</b>	40,341,506.89
<b>2</b>	<b>Kunyanyua jengo (super structure)</b>	
<b>A</b>	<b>Kusuka nondo katika</b>	
i	Nguzo wima Kutoka kwenye jamvi hadi katika nguzo mlalo za katikati (intermediate beam) na kutoka intermediate beam hadi kwenye nguzo mlalo za kupokea paa ( roof beam)	1,458,706.495
ii	Katika Nguzo mlalo za kati (intermediate beam ) na nguzo malalo za kupokea paa (Roof beam)	890,128.539
iii	Katika sakafu ya baraza la mbele (first floor at entry)	191,501.757
iv	Katika Ramp, coping ya juu kwenye nguzo za urembo	429,105.789
		2,969,442.581
<b>B</b>	<b>Kufunga na kuondoa mbao</b>	
i	Katika nguzo wima Kutoka kwenye jamvi hadi katika nguzo mlalo za katikati (intermediate beam) na kutoka intermediate beam hadi kwenye nguzo mlalo za kupokea paa ( roof beam)	1,088,722.953
ii	Katika Nguzo mlalo za kati (intermediate beam ) na nguzo malalo za kupokea paa (Roof beam)	3,489,587.577
iii	Katika sakafu ya baraza la mbele (first floor at entry).	383,003.515
iv	Katika Ramp, coping ya juu kwenye nguzo za urembo	542,588.312
		5,503,902.36
<b>C</b>	<b>Kumwaga zege</b>	
i	Katika nguzo wima Kutoka kwenye jamvi hadi katika nguzo mlalo za katikati (intermediate beam) na kutoka intermediate beam hadi kwenye nguzo mlalo za kupokea paa ( roof beam)	861,757.908
ii	Katika Nguzo mlalo za kati (intermediate beam ) na nguzo malalo za kupokea paa (Roof beam)	1,347,604.950
iii	Katika sakafu ya baraza la mbele (first floor at entry).	443,291.105
iv	Katika Ramp, coping ya juu kwenye nguzo za urembo	574,505.272
		3,227,159.24



Na	AINA YA KAZI	BEI YA UFUNDI
A	Ujenzi wa kuta	
i	Katika kuta za nje	4,681,154.667
ii	Katika kuta za ndani na kuta za urembo kuzunguka jengo na juu ya paa	2,482,430.181
		7,163,584.857
	<b>JUMLA YA KUNYANYUA JENGO (SUPERSTRUCTURE)</b>	18,864,088.441
3	<b>Kuezeka (Roof structure)</b>	
i	Kutengeneza kenchi za mbao kwa kufuata mchoro	5,745,021.719
ii	Kupandisha kenchi za mbao kwenye jengo	1,149,010.544
iii	kuezeka	4,744,636.590
iv	Kufunga matega maji (gutters & downpipes) kuzunguka jengo	861,737.1908
	<b>JUMLA NDOGO KUEZEKA</b>	12,550,457.761
4	<b>MILANGO</b>	
i	Kufitisha fremu za milango	1,035,528.021
iii	Kuweka urembo wa pembeni mwa fremu za mbao (Architrave)	276,613.649
	<b>JUMLA NDOGO MILANGO</b>	1,312,141.671
5	<b>MADIRISHA</b>	
i	Kufitisha madirisha ya chuma (grill)	1,276,678.382
	<b>JUMLA NDOGO MADIRISHA</b>	1,276,678.382
6	<b>UMALIZIAJI (Finishing)</b>	
A	<b>Upigaji wa lipu pamoja kutengeneza wa koplo</b>	
i	Nje ya jengo	3,830,035.146
ii	Ndani ya jengo	2,078,148.700
iii	Kwenye kuta za urembo, Nguzo za mbele, kwenye coping, kwenye dari ya zege (concrete ceiling) at entry	1,150,475.308
		7,058,659.150
A	Uwekaji wa sakafu ya kupokea vigae	3,120,769.378
ii	Uwekaji wa sakafu ya kupokea EPOXY floor.	1,449,010.544
iii	Uwekaji wa vigae pamoja na grout katika sakafu (floor tiles)	4,893,933.797
iv	Uwekaji wa vigae pamoja grout katika kuta za vyooni na mabafuni (wall tiles)	1,007,157.390
v	Uwekaji wa floor EPOXY FLOOR	2,010,768.452
		12,181,639.161
B	<b>DARI</b>	
i	Ufungaji wa mbao za dari (brandering)	3,125,296.606
ii	Ufungaji wa gypsum board pamoja na mikanda yake	4,681,154.667
		7,806,450.671
	<b>JUMLA NDOGO YA UMALIZIAJI JENGO (FINISHING)</b>	27,046,749.139



Na	AINA YA KAZI	BEI YA UFUNDI
<b>7</b>	<b>Rangi na Mapambo (painting &amp; Decorations)</b>	
<b>A</b>	Kupaka rangi ,mikono mitatu pamoja na Skimming katika	
i	Nje ya jengo	3,900,961.723
ii	Ndani ya jengo	2,759,043.837
iii	Kwenye kuta za urembo za jengo, kwenye coping, kwenye ceiling ya zege (at entry) na kwenye ceiling ya gypsum board na mikanda yake.	461,022.749
iv	Dari	2,665,699.096
		9,786,727.401
<b>B</b>	<b>Kupaka rangi ,mikono mitatu katika</b>	
i	Msingi wa nyumba	173,770.113
ii	Fascia board na roof vent	258,527.372
iii	Madirisha ya chuma (grill)	578,505.272
		1,006,802.757
	<b>JUMLA NDOGO YA RANGI NA MAPAMBO</b>	10,793,530.161
<b>8</b>	<b>UMEME &amp; FIRE (electrical installation)</b>	
i	Usukaji wa umeme awamu ya kwanza (conduit na box) hii ikujumuisha na pointi za DP za AC,data etc, pamoja na uwekaji wa panel zote kulingana na mchoro wa engineer wa services	2,010,768.432
ii	Usukaji wa umeme awamu ya pili (2 <sup>nd</sup> fix) ufungaji wa vifaa vyote vya umeme (fittings)	4,165,163.221
	<b>JUMLA NDOGO UMEME &amp; FIRE(electrical installation)</b>	6,175,931.653
<b>9</b>	<b>AC INSTALLATION</b>	
i	Uwekaji wa pipe za AC (Copper pipe) awamu ya kwanza.	689,406.326
ii	Ufungaji wa indoor na outdoor machines za AC pamoja na vifaa vingine vya AC kulingana na mchoro	2,757,625.305
	<b>JUMLA NDOGO AC INSTALLATION</b>	3,447,031.631
<b>10</b>	<b>MIFUMO YA MAJI SAFI NA MAJI TAKA (WATER SUPPLY AND SEWERAGE SYSTEM).</b>	
I	Ufungaji bomba awamu ya kwanza (kuchimbi bomba) 1 <sup>st</sup> fix	3,837,873.835
ii	Ufungaji wa vifaa vya bomba (kama vyoo,HWB,shattaf,water taps,soap holder nk)	4,452,415.857
iii	Uchimbaji wa wa mashimo ya maji taka (septic and soak away tanks)	2,154,399.776
iv	Ujenzi wa mashimo ya taka pamoja na chemba zake,kumwaga zege na kufanyia finishings.	2,441,677.405
	<b>JUMLA NDOGO MIFUMO YA MAJI SAFI NA MAJI TAKA</b>	12,886,331.873



[illegible]



**9.MCHANGANUO WA MAKADIRIO YA  
VIFAA VYA UJENZI**

*AP*

ITEM	DESCRIPTION	QTY	UNIT	RATE	AMOUNT
	<b>ELEMENT NO.1- SUBSTRUCTURE</b>				
	<b>ALL PROVISIONAL</b>				
a	200mm hardcore stone - (4.5 m3 Lorry)	43	Trips	80,000	3,440,000
b	Sand blinding	9	Trips	55,000	495,000
c	soil sterilization over hardcore bed.	840	M <sup>2</sup>	500	420,000
d	Earth filling selected imported pure sand; well compacted in 300mm thick layers; to make up levels under the floors	20	Trips	55,000	1,100,000
e	Load up surplus excavated materials and remove from site	20	Trips	55,000	1,100,000
	<b>CONCRETE WORK</b>				
f	<u>50mm blinding 1:4:8</u>				
	cement - 50 Kgs 42.5	109	Bags	22,000	2,398,000
g	sand	5	Trips	55,000	275,000
h	aggregates (1/2")	10	Trips	270,000	2,700,000
	<u>Plain concrete grade '20' (1:2:4)</u>				
	<u>150mm over site bed</u>				
j	cement - 50 Kgs 42.5	1,194	Bags	22,000	26,268,000
k	sand	19	Trips	55,000	1,045,000
l	aggregates- 1/2"	38	Trips	270,000	10,260,000
	<b>Reinforcement</b>				
m	Fabric reinforcement to BS 4483 ref. A252 weighing 3.95 kg per square metre laid in bed and ramps	995	M <sup>2</sup>	4,200	4,179,000
	To Collection				53,680,000



ITEM	DESCRIPTION	QTY	UNIT	RATE	AMOUNT
	<b>Reinforced concrete grade 20 to:-</b>				
	<u>Ground beams</u>				
a	cement - 50 Kgs 42.5	216	Bags	22,000	4,752,000
b	sand	4.00	Trips	55,000	220,000
c	aggregates- 3/4"	7.00	Trips	270,000	1,890,000
d	Y16 Reinforcement bars;12 metres long	199	No	48,000	9,552,000
e	Y8 Reinforcement bars;12 metres long	295	No	16,000	4,720,000
f	Binding wires	15	Kgs	3,500	52,500
	<u>Columns bases &amp; starter columns</u>				
g	cement - 50 Kgs 42.5	36	Bags	22,000	792,000
h	sand	1.00	Trips	55,000	55,000
j	aggregates- 3/4"	2.00	Trips	270,000	540,000
	<u>Reinforcement bars;12 metres long</u>				
k	Y12 Reinforcement bars;12 metres long	40	No	28,000	1,120,000
l	Y8 Reinforcement bars;12 metres long	25	No	16,000	400,000
m	Binding wires	6	Kgs	3,500	21,000
	To Collection				24,114,500



ITEM	DESCRIPTION	QTY	UNIT	RATE	AMOUNT
	<b><u>Walling</u></b>				
	<b><u>Solid cement sand blocks to B.S 2028 type 'A' bedded and jointed in cement and sand mortar (1:4)</u></b>				
a	6" cement and sand block- 5Mpa (230mm thick) <u>block making mortar</u>	8,527	No	1,500	12,790,500
b	cement : 50 Kgs 42.5	244	Bags	22,000	5,359,829
c	sand	8	Trips	55,000	440,000
d	SIKAFLEX-PRO 2HP ISOLATION JOINT; for expansion joint sealant applied in accordance to Manufacturer's specifications to 150mm deep concrete slab	6	Pcs	42,000	252,000
	<b><u>Damp Proof Courses</u></b>				
e	DPM Sheets 500gauge	877	M2	2,700	2,367,900
f	dpc ;230mm wide	7	Roll	80,000	560,000
g	Allow cost for construction of reinforced ramps as per project manager's instructions <b><u>15mm thick plaster to plinth level (1:4)</u></b>	4	No	200,000	800,000
h	cement - 50 Kgs 42.5	15	Bags	22,000	330,000
j	sand for mortar	1.0	Trips	55,000	55,000
